




**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA
(PPRA)**

**MWONGOZO WA UNUNUZI KWA KUTUMIA
FEDHA ZA MFUKO WA KUCHOCHEA MAENDELEO YA JIMBO**

FEBRUARI, 2025

Tarehe ya kuanza kutumika: 4 Februari, 2025

**MWONGOZO WA UNUNUZI KWA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA
KUCHOCHEA MAENDELEO YA JIMBO**

Imeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Cheo Mkurugenzi Mkuu	Sahihi 	Tarehe 3 Februari, 2025
--	--------------------------------	---	--

Issued by:

Director General,
Public Procurement Regulatory Authority,
Tambukareli Dodoma,
3 Ununuzi Street,
P. O. Box 2865,
41104 Dodoma,
TANZANIA
Email Address: dg@ppra.go.tz
Phone: +255 (0) 26 296 3854
Website: <https://www.ppra.go.tz>

YALIYOMO

ORODHA YA VIFUPISHO	iv
TAARIFA ZA UDHIBITI WA NYARAKA	v
SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	1
Utangulizi	1
SEHEMU YA PILI: VIFUNGU VYA AWALI	1
Jina la Mwongozo	1
Kusudi la Mwongozo huu	1
Matumizi ya Mwongozo	2
Tafsiri	2
SEHEMU YA TATU: MISINGI YA JUMLA	4
Manufaa ya Mfuko	4
Sifa za Wazabuni	4
SEHEMU YA NNE: MPANGO WA UNUNUZI	5
Maandalizi ya Mpango wa Mwaka wa Ununuzi	5
Ushirikishwaji wa jamii ya Halmashauri husika katika zabuni	6
SEHEMU YA SITA: UTARATIBU WA UNUNUZI	6
Njia za Ununuzi	6
Nyaraka za Zabuni Zitakazotumika	7
Matumizi ya Mfumo wa NeST	7
Mwaliko wa Zabuni	7
Tathmini na utoaji Tuzo	7
Utatuzi wa migogoro	8
Dhamana	8
Matumizi ya Rasilimali za ndani	8
SEHEMU YA VII: MAPITIO YA MWONGOZO	9
Mapitio ya Mwongozo	9
JEDWALI	10

ORODHA YA VIFUPISHO

- NeST - National Electronic Procurement System of Tanzania
- SUU - Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410
- KUU - Kanuni za Ununuzi wa Umma, Tangazo Na. 518 la Mwaka 2024

TAARIFA ZA UDHIBITI WA NYARAKA

Jina la Nyaraka	Mwongozo wa Ununuzi kwa Kutumia Fedha za Mfuko wa Jimbo, 2025
Toleo	Toleo la Kwanza, Januari 2025
Namba ya Nyaraka	PPRA/PSCD/MPS/25/13
Jukumu	Menejimenti, Taasisi Nunuzi, Makundi Maalum na Wazabuni
Imeandaliwa na	Menejimenti
Idhini, Toleo la Kwanza	Bodi, Januari 2025
Matumizi	Taasisi Nunuzi, Wazabuni, Makundi Maalum na Menejimenti
Kusudi	Kusudi kuu la Mwongozo huu ni kutoa utaratibu wa ununuzi kwa kutumia Fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo.
Ni sehemu ya	Miongozo ya Ununuzi wa Umma
Nyaraka Nyingine zinazohusishwa	Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Kanuni za Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023
Usambazaji	Bodi, Menejimenti, Taasisi Nunuzi, Makundi Maalum, Wazabuni na Afisa Masuuli



		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI
1.	Utangulizi	<p>1.1 Kwa mujibu wa Kifungu cha 10(f) na 130 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imepewa jukumu la kutoa miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa malengo au majukumu chini ya Sheria hii.</p> <p>1.2 Kwa mujibu wa Kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo Sura ya 96 (Kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2020) ununuzi wa bidhaa, huduma na kazi za ujenzi kwa kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo utatekelezwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura Na. 410.</p> <p>1.3 Kufuatia mahitaji ya kisheria yaliyotajwa hapo juu, Mamlaka inatoa Mwongozo huu kwa ununuzi wote utakaotekelezwa kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Jimbo.</p>
		SEHEMU YA PILI: VIFUNGU VYA AWALI
2.	Jina la Mwongozo	Mwongozo huu utajulikana kama Mwongozo wa Ununuzi kwa kutumia Fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2025.
3.	Kusudi la Mwongozo huu	<p>3.1 Kusudi kuu la Mwongozo huu ni kutoa utaratibu wa ununuzi kwa kutumia Fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo.</p> <p>3.2 Kusudi Maalum la Mwongozo huu ni:</p> <ul style="list-style-type: none"> a) Kurahisisha uelewa wa utaratibu wa kusimamia ununuzi kwa kutumia Fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo; na b) Kuziwezesha Halmashauri kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na

		sheria ya Mfuko wa Jimbo Sura ya 96.
4.	Matumizi ya Mwongozo	4.1 Mwongozo huu utatumika katika kila jimbo ndani ya Halmashauri pale linapotumia fedha za Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo.
5.	Tafsiri	<p>5.1 Katika Mwongozo huu, isipokuwa pale muktadha utakapohitaji vinginevyo: -</p> <p>“Afisa masuuli” maana yake ni afisa wa umma aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha za Umma au afisa wa umma aliyeteuliwa kwa sheria nyingine yoyote kusimamia fungu au ruzuku na kuwajibika kwa fedha zote zilizotumika kutoka katika fungu hilo au ruzuku;</p> <p>“Mamlaka” maana yake ni Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 8 cha sheria ya ununuzi wa umma Sura ya 410;</p> <p>“Kamati” maana yake ni Kamati ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo</p> <p>“Jamii” maana yake ni wakazi wanaoishi ndani ya Halmashauri husika;</p> <p>“Mzabuni” kwa madhumuni ya mwongozo huu maana yake ni makundi ya kijamii, makundi maalum na wazabuni walio ndani ya Halmashauri wanaoshiriki au wanaokusudia kushiriki kwenye mchakato wa ununuzi kwa lengo la kuwasilisha zabuni kwa ajili ya kuingia mkataba na Halmashauri;</p> <p>“Mkataba wa ununuzi” maana yake ni leseni, kibali</p>

		<p>au idhini nyingine iliyotolewa na taasisi ya umma au makubaliano yaliyoingiwa baina ya taasisi ya umma na muuzaji wa bidhaa, mkandarasi, au mshauri elekezi yanayotokana na utaratibu wa ununuzi kwa ajili ya ujenzi au kazi nyingine zinazohusiana na ujenzi au kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa zozote au utoaji wa huduma;</p> <p>“Taratibu za ununuzi” maana yake ni taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na taasisi nunuzi au mamlaka yoyote ya kutoa idhini inapojihusisha katika ununuzi;</p> <p>“Mchakato wa ununuzi” maana yake ni hatua zinazofuatana katika mzunguko wa ununuzi zinazojumuisha kupanga, kuchagua utaratibu, hatua za kuomba ofa kutoka kwa wazabuni, kupima na kutathmini ofa hizo, utoaji wa tuzo ya mkataba na usimamizi wa mkataba;</p> <p>“Kanuni” maana yake ni Kanuni za Ununuzi wa Umma, (TS.Na. 518) la 2024 kama ilivyorekebishwa;</p> <p>“Sheria” maana yake ni Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Sheria ya Mfuko wa Jimbo Sura ya 96,</p> <p>"Kundi Maalum" ni muunganiko wa watu wenye nia ya pamoja ya kushiriki katika ununuzi wa umma kama kikundi cha wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu;</p> <p>“Ununuzi” maana yake ni kununua, kupanga,</p>
--	--	---

		kukodisha, kununua kwa kukodisha au kupata bidhaa, kazi za ujenzi au huduma yeyote kwa taasisi nunuzi na inajumuisha kazi zote zinazohusisha upatikanaji wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma ikijumuisha kutambua na kuandaa mahitaji, uchaguzi na mwaliko wa wazabuni, maandalizi ya mikataba, tuzo na usimamizi wa mikataba;
		SEHEMU YA TATU: MISINGI YA JUMLA
6.	Manufaa ya Mfuko	<p>6.1 Mwongozo unaweka misingi ya utekelezwaji wa sheria, kanuni na taratibu zitakazozingatiwa ili kutoa mchango unaokusudiwa katika Taifa;</p> <p>6.2 Halmashauri zitahakikisha kuwa fedha za Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo zinalenga kuwanufaisha wananchi wa jimbo husika ndani ya Halmashauri;</p> <p>6.3 Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha zinapotangaza zabuni zinaweka kipaumbele kwa wazabuni walio ndani ya jimbo la Halmashauri husika kwanza.</p>
7.	Sifa za Wazabuni	<p>Kwa madhumuni ya kufuzu kushiriki katika michakato ya ununuzi wa umma kwa kutumia fedha za Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo, makundi ya kijamii, makundi maalum na wazabuni walio ndani ya jimbo la Halmashauri wanaokusudia kushiriki katika ununuzi wa umma watapaswa kuwa na sifa zifuatazo:</p> <p><u>A: Makundi ya Kijamii / Maalum</u></p> <p>(a) Kuwa wanafanya shughuli zao ndani ya jimbo la Halmashauri husika;</p> <p>(b) Wamesajiliwa na kutambuliwa na taasisi inayosimamia makundi maalumu husika;</p>

		<p>(c) Wameingizwa katika rejesta maalumu ya Mamlaka baada ya kuwasilishwa na taasisi inayosimamia makundi maalumu husika;</p> <p>(d) Yana angalau asilimia sabini ya uanachama wa wanachama wanaounda kundi hilo na linaongozwa kwa asilimia mia moja na kundi maalumu husika; na</p> <p>(e) Lina sifa muhimu, uwezo, rasilimali za kutosha, vifaa na miundombinu ya kuuza bidhaa, kazi za ujenzi na huduma zinazotarajiwa kununuliwa.</p> <p>(f) Kwa madhumuni ya Mwongozo huu, watakuwa ni watanzania wazawa kwa asilimia mia moja na wakazi wa jimbo la Halmashauri husika.</p> <p><u>B: Wazabuni</u></p> <p>(a) Wawe wanafanya shughuli zao ndani ya jimbo la Halmashauri husika;</p> <p>(b) Wawe wamesajiliwa kwenye mfumo wa NeST na kuwa na sifa zote za usajili kwa zabuni wanazotaka kushiriki;</p> <p>(c) Kwa madhumuni ya Mwongozo huu, watakuwa ni watanzania wazawa kwa asilimia mia moja na wakazi wa jimbo la Halmashauri husika.</p>
		SEHEMU YA NNE: MPANGO WA UNUNUZI
8.	Maandalizi ya Mpango wa Mwaka wa Ununuzi	<p>8.1 Miradi yote iliyoidhinishwa na Kamati itajumuishwa kwenye mpango wa ununuzi wa mwaka wa halmashauri husika</p> <p>8.2 Pale ambapo miradi iliyoidhinishwa na Kamati haijajumuishwa kwenye mpango wa ununuzi uliodhinishwa, idhini ya afisa masuuli itatolewa kwa kujumuisha mahitaji hayo kwenye mpango wa ununuzi au kuwasilisha maombi ya idhini kwa ununuzi mahususi ambao haujajumuishwa kwenye mpango wa</p>

		ununuzi.
9.	Ushirikishwaji wa jamii ya Halmashauri husika katika zabuni	<p>9.1. Kwa mujibu wa Kifungu cha 19 (1) cha Sheria ya Mfuko wa fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo, Sura Na. 96, miradi yote au ununuzi wote chini ya Sheria ya Mfuko wa fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo itatekelezwa kwa misingi ya ushirikishwaji wa jamii ili faida zitakazopatikana na ununuzi huo ziwanufaishe wanajamii wengi wa Halmashauri husika.</p> <p>9.2. Halmashauri zinaweza kuandaa zabuni ya vifaa/bidhaa, kazi za ujenzi au huduma katika loti ili kuhakikisha ushiriki mkubwa wa wazabuni kwenye zabuni ndani ya jimbo.</p>
SEHEMU YA SITA: UTARATIBU WA UNUNUZI		
10.	Njia za Ununuzi	<p>10.1. Njia za ununuzi zitakazotumika chini ya Mwongozo huu zitajumuisha:</p> <ul style="list-style-type: none"> a) Njia ya Ushindani wa zabuni ndani ya Wilaya au Jimbo husika; b) Njia ya ununuzi uliozuiliwa kwa wazabuni wachache; c) Njia ya ununuzi wa thamani ndogo usiotumia fedha taslimu; d) Njia ya ununuzi wa thamani ndogo unaotumia fedha taslimu; e) Njia ya ununuzi ya Kotesheni Shindani; na f) Njia ya ununuzi kutoka kwa mzabuni mmoja. <p>10.2. Uchaguzi wa njia utategemea thamani na mazingira ya ununuzi unaotarajiwa kufanyika;</p>

		10.3. Uchaguzi wa njia utazingatia vigezo vya matumizi ya njia husika vilivyoainishwa katika Kanuni za Ununuzi wa Umma
11.	Nyaraka za Zabuni Zitakazotumika	Halmashauri zitatumia nyaraka sanifu za zabuni zinazopatikana kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma.
12.	Matumizi ya Mfumo wa NeST	Halmashauri zitatumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) katika ununuzi unaotumia Fedha za Mfuko wa kuchochea maendeleo wa Jimbo.
13.	Mwaliko wa Zabuni	<p>13.1 Mwaliko wa zabuni zinazotumia fedha za Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo utatolewa kwa wazabuni waliosajiliwa kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi Umma (NeST).</p> <p>13.2 Wazabuni watakoalikwa katika zabuni zilizotolewa na Halmashauri kwa kutumia fedha za Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo watatoka kwenye jimbo husika ndani ya halmashauri.</p> <p>13.3 Pale ambapo Halmashauri imekosa wazabuni au hajaipokea zabuni au haijapata mzabuni mwenye sifa kutoka kwa wazabuni ndani ya jimbo, kwa idhini ya Kamati, zabuni husika itatangazwa upya kwa wazabuni waliopo kwenye majimbo mengine ndani ya halmashauri au mkoa ilipo Halmashauri.</p>
14.	Tathmini na utoaji Tuzo	14.1 Tathmini ya zabuni katika ununuzi unaotumia fedha za Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo itafanyika kwa kuzingatia miongozo ya Tathmini ya zabuni iliyotolewa na Mamlaka.

		<p>14.2 Kwa mujibu wa kifungu cha 15 (2) cha Sheria ya Mfuko wa fedha za kuchochea maendeleo ya Jimbo, kabla ya utoaji wa tuzo ya mkataba, Afisa masuuli atawasilisha kwenye Kamati, mapendekezo ya tuzo ya mkataba inayotakiwa kutolewa kwa ajili ya kupata ridhaa ya Kamati hiyo.</p> <p>14.3 Ridhaa itakayotolewa na Kamati itatolewa katika fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Mwongozo huu.</p>
15.	Utatuzi wa migogoro	Endapo kutatokea migogoro au kutoelewana baina ya Afisa masuuli na Kamati, Afisa masuuli atawasilisha suala hilo kwa Mamlaka kwa ajili ya maelekezo.
16.	Dhamana	<p>16.1. Aina ya dhamana ya zabuni itakayotumika kwa ununuzi unaohusisha Mfuko wa Jimbo itakuwa ni Tamko la Dhamana la Zabuni.</p> <p>16.2. Kabla ya kuingia mkataba wa ununuzi na Halmashauri, wazabuni watawasilisha Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba kwa mikataba ya kazi za ujenzi yenye thamani isiyozidi shilingi milioni mia tano na kwa mikataba ya huduma na bidhaa yenye thamani isiyozidi shilingi milioni mia mbili;</p> <p>16.3. Wazabuni watawasilisha dhamana ya utekelezaji wa mkataba ikiwa katika muundo wa dhamana ya benki au bima kwa mkataba unaozidi thamani iliyoainishwa katika kifungu cha 16.2 cha Mwongozo huu.</p>
17.	Matumizi ya Rasilimali za	17.1. Halmashauri inaweza kutekeleza mradi wa ujenzi kwa utaratibu wa Matumizi ya Rasilimali za Ndani

	ndani	<p>(Force Account) endapo Halmashauri ina wataalam na vifaa vya kutekeleza kazi hiyo ya ujenzi.</p> <p>17.2. Utekelezaji wa mradi kwa utaratibu wa Matumizi ya Rasilimali za Ndani utazingatia Mwongozo wa utekelezaji miradi kwa utaratibu wa Matumizi ya Rasilimali za Ndani wa mwaka 2025 uliotolewa na Mamlaka.</p>
SEHEMU YA VII: MAPITIO YA MWONGOZO		
18.	Mapitio ya Mwongozo	Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu au pale itakapohitajika.

JEDWALI

MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA MAENDELEO YA MFUKO WA JIMBO

KIKAO No. [Taasisi nunuzi aininisha kikao hiki cha ngapi] cha [Mwaka wa fedha]
[Tarehe, Mwezi na Mwaka]

Dhumuni la kikao: [weka jina/maelezo ya mradi]

1.0 UTANGULIZI

1.1 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya mfuko wa maendeleo wa Jimbo la halmashauri ya [weka jina la PE] kwa ajili ya [Mwaka wa fedha] Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizi zitatumika kulipia malipo yanayostahiki chini ya Mkataba wa [weka jina la mradi na Namba ya Mkataba/Zabuni].

2.0 MAELEZO YA UNUNUZI

2.1 Kamati imepokea maombi ya kuidhinisha ununuzi/michakato ya ununuzi [Maelezo yanaweza kujumuisha michakato yote iliyofanywa kabla ya kutafuta idhini hii. Eleza kama nukuu/zabuni ziliitwa, tathmini iliyofanywa n.k kulingana na maendeleo yaliyofikiwa. Unaweza kuingiza jedwali ili kufupisha maelezo yako inapohitajika. Ambatisha hati yoyote ili kuhifadhi nakala ya maelezo yako]

2.2 Kamati ya maendeleo ya Mfuko wa Jimbo la [Taja jina la halmashauri] kimepokea mahitaji kutoka kwa [weka jina la idara ya mtumiaji] kuomba idhini ya ununuzi wa [weka jina la mradi]. Maelezo ya mahitaji yamefupishwa hapa chini:-

S/N	Maelezo ya huduma[Item Description]	Jina la mzabuni	Kiasi
1			
2			

2.3 Kwa kuzingatia maombi yaliyowasilishwa, kamati haina pingamizi au inapingamizi kwa kutolewa kwa tuzo ya mkataba.

Mwenyekiti wa kamati

Kamati ya maendeleo ya mfuko wa jimbo la halmashauri [taja jina la halmashauri]

[Tarehe]

S/N	Jina	Cheo	Nimekubali/Sijakubali	Sahihi	Tarehe
1		Mwenyekiti			
2		Mjumbe			
3		Mjumbe			
4		Mjumbe			
5		Mjumbe			
6		Mjumbe			
7		Mjumbe			